

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA RUKWA

Telegraphic: "REGCOM"

Simu. No:0252802137/2802138/2802144

Fax No. (025) 2802217/2802318

E-mail:ras.rukwa@tamisemi.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA,
P. O. Box 128,
SUMBAWANGA.

03 Agosti 2016

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI RUKWA

Ninayo mambo machache muhimu nataka kusema kwa manufaa ya Wananchi wa Mkoa wangu wa Rukwa.

1. Ninalo jukumu la kuhakikisha kwamba amani na utulivu inadumishwa katika Mkoa mzima. Vivyo hivyo Wakuu wa Wilaya wanalo jukumu hilo.

- Wajibu Serikali yoyote ni kuwalinda wananchi wake.
- Hivyo, matarajio ya wananchi kwa Serikali yao ni kuwa itawahakikishia usalama wao na mali zao wakati wote ili waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi, kijamii na kimaisha bila hofu. Kwa sababu hiyo Ulinzi na Usalama ni hitajio muhimu sana katika maisha ya kila siku ya Wananchi na Nchi kwa ujumla.
- Amani na utulivu ni mtaji mkubwa sana kwa mwananchi kufanya shughuli za kuendesha maisha yao na maendeleo.

Nisingependa kuona au kuruhusu rasilimali muda ambao kila mtu anahitaji unatumika vibaya kwa mikutano ya hadhara na maandamano ambayo sio wakati wake. Huu ni wakati wa kuwaacha wachapakazi wa Rukwa kujikita kwenye uzalishaji mali.

- Natambua kwamba Mkoa wa Rukwa una Majimbo matano ya Uchaguzi na Kata 64 zenye Madiwani waliochaguliwa kidemokrasia katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 2015 ukihusisha Vyama vyao vya Siasa.
- Wawakilishi hao sasa wana haki na wajibu wa kukutana na wananchi hadharani ama ndani kuhimiza maendeleo na kuchapa kazi na siyo vinginevyo. Natumaini Waheshimiwa Wabunge na Madiwani katika Mkoa wa Rukwa wanafanya hivyo kwa kuzingatia sheria zilizotungwa na Bunge ikiwamo ile Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi sura 322.
- Wananchi katika Mkoa wa Rukwa wanatambua na kuenzi Amani na Utulivu wao. Nina kila sababu ya kushikamana na kushirikiana nao na ndivyo wanavyofanya Wakuu wa Wilaya kulinda mtaji huo muhimu ili wapate nafasi nzuri ya kuchapa kazi kwa manufaa yao.
- Rukwa inawakaribisha wale wenye uwezo wa kuanzisha Viwanda vya kuongeza thamani mazao ya Kilimo na Mifugo kujenga vyuo, kuboresha mazingira na siyo vinginevyo.

- Natoa rai kwa Viongozi wa Kada mbalimbali, wazee mashuhuri, Wazee wa mila, Viongozi wa Madhehebu ya dini, Vijana, kina Baba na kina Mama sote tusimamie amani na utulivu.
- Navitaka vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama vitimize majukumu yao kikamilifu, ili kulinda Amani na Utulivu kwa nguvu zao zote kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu kila dakika ya utendaji wao.

2. Usalama wa Chakula

Tumeanza kusikia baadhi ya maeneo nchini yana upungufu wa chakula. Hivi sasa Mkoa wa Rukwa upo katika msimu wa mavuno. Mavuno yanatarajiwa kuwa kiasi cha tani 954,416.6, Mahitaji ya Mkoa ni tani 369,523.2. Natoa tahadhari kila kaya kuhifadhi chakula cha kutosha na kuuza ziada inapokuwa lazima. Wakuu wa Wilaya na Wabunge wahimize na kusimamia jambo hili.

3. Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula Mkoa wa Rukwa wameidhinishiwa kununua tani 16,000 kwa masharti kwamba waende kwenye vijiji walipo wakulima.

Zelote Stephen Zelote
**MKUU WA MKOA
RUKWA**